

WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA

Tarehe: 27 April, 2022



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MUDA

Bodi ya Korosho Tanzania ni Taasisi ya umma iliyoko chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009. Bodi hii imekasimiwa jukumu la kusimamia maendeleo ya zao la korosho katika ngazi zote za uzalishaji, ubanguaji/usindikaji, masoko na utafiti ili kuhakikisha kuwa zao la korosho linatoa mchango wake katika kuinua pato la mkulima wa zao hili na Taifa kwa ujumla.

1. WASIMAMIZI WA MASHAMBA YA KOROSHO - MANYONI

A. SIFA ZA WAOMBAJI

- (a) Awe Mtanzania na umri kuanzia Miaka 18 - 40;
- (b) Awe amehitimu kidato cha IV na kufaulu masomo ya Kiswahili na Kiingereza;
- (c) Awe na Cheti cha Stashahada ya Kilimo au sifa zinazofanana na hizo kutoka Chuo kinachotambulika na serikali
- (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (e) Awe Mkazi wa Mkoa wa Singida na maeneo mengine ya jirani

B. MAJUKUMU YA KAZI YA WASIMAMIZI WA MASHAMBA YA KOROSHO

- (a) Kushirikiana na wakulima kuendesha mashamba darasa na mashamba ya majaribio.
- (b) Kutembelea wakulima na vikundi vya wakulima katika mashamba yao ya korosho na kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya mbinu bora za kisasa za kilimo biashara.
- (c) Kuwafundisha na kuwaeleza wakulima juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu, mbolea, madawa na zana za kilimo.
- (d) Kukusanya na kutunza takwimu za hali ya kilimo cha Korosho.
- (e) Kutoa taarifa juu ya dalili za kuwepo visumbufu wa Korosho.
- (f) Kuandaa na kutumia daftari la kilimo katika kutekeleza majukumu ya kila siku.
- (g) Kuandaa taarifa ya utekelezaji ya kila mwezi na kuiwasilisha Tawi la Manyoni.

(h) Kusimamia ubora wa zao la Korosho kuanzia shambani hadi inapouzwa sokoni

Mshahara

Mshahara wa kazi hii kwa mwezi ni Tsh 450,000/=

Ajira hii ni ya mkataba wa miezi Sita sio ya kudumu.

Maombi yote yatumwe kwa anuani hii kabla ya tarehe 11.05.2022 saa 10:00 jioni.

MKURUGENZI MKUU,
BODI YA KOROSHO TANZANIA,
S.L.P 533,
MTWARA

info@cashew.go.tz